# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

## TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI-SEPTEMBA) MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWENYE KIKAO CHA TAREHE 06/11/2021


**IMEANDALIWA NA:**
OFISI YA MKURUGENZI,
HALMASHAURI YA MANISPAA ILEMELA,
S.L.P 735,
**ILEMELA-MWANZA.**


**Novemba, 2021**

Scanned with CamScanner

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

**Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe,**

**Baraza la Madiwani.**

## TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA) MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWENYE KIKAO CHA TAREHE 06/11/2021

### 1.0. UTANGULIZI

**Mhe. Mwenyekiti**, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa taarifa ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya mwaka. Hivyo, taarifa hii itagusa maeneo yafuatayo:-

i. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maegesho ya malori na stendi ya mabasi Nyamhongolo
ii. Taarifa ya Matokeo ya Mtihani wa Darasa la Saba wa Mwaka 2021
iii. Taarifa ya Mtihani wa Kidato cha Pili na cha nne kwa Mwaka 2021
iv. Taarifa ya Mapokezi wa Fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Kituo cha Afya Kayenze na ujenzi wa miundo mbinu ya vyumba vya madarasa katika shule za sekondari.
v. Taarifa ya kuwapanga machinga/wafanyabiashara ndogondogo katika maeneo rasmi
vi. Taarifa ya Uzinduzi wa Kampeni ya Usafi na Mazingira katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela
vii. Taarifa ya kuwajengea uwezo Waheshiwa Madiwani na Watendaji wa Kata.
viii. Taarifa ya Uhamasishaji na Uchanjaji wa Chanjo ya UVIKO-19

Scanned with CamScanner

## 2.0. UFAFANUZI WA TAARIFA

### 2.1 Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati Nyamhongolo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri inaendelea na utekelezaji wa miradi miwili ya kimkakati ya ujenzi wa maegesho ya malori na ujenzi wa stendi ya mabasi katika eneo la Nyamhongolo kwa gharama ya Tsh. 27,095,103,464.00. Hadi sasa miradi hiyo yote miwili imefikia utekelezaji kwa wastani wa asilimia 91% na Halmashauri imepokea jumla ya Tsh. 17,359,943,691.54 ambazo tayari fedha zote zimelipwa kwa Mkandarasi pamoja na Mtaalam Mshauri. Maendeleo ya miradi yote kwa ujumla ni mazuri na mkandarasi yupo anaendelea na kazi kwa kasi nzuri inayoashiria kuwa anaweza kumaliza miradi yote kwa muda uliopangwa endapo mtiririko wa fedha utaenda vizuri. Miradi yote miwili inatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 20 January, 2021 kwa mujibu wa mkataba.

### 2.2 Taarifa ya Matokeo ya Mtihani wa Darasa la Saba wa Mwaka 2021

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Baraza la Mitihani lilitangaza matokeo ya mtihani wa Darasa la saba wa mwaka 2021 ambapo katika shule za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela jumla ya wanafunzi 10,748 wakiwemo Wavulana 5179 na Wasichana 5569 walifanya mtihani huo. Katika matokeo ya mtihani huo wanafunzi 10,393 wakiwemo Wavulana 5354 na Wasichana 5039 sawa na asilimia 96.7 walifaulu kwa daraja A-C na Halmashauri imeshika nafasi ya pili Kimkoa na nafasi ya 7 Kitaifa.

### 2.3 Taarifa ya Mtihani wa Kidato cha Pili na cha Nne kwa Mwaka 2021

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mnamo tarehe 01 – 10/11/2020, zoezi la mitihani kwa wanafunzi wa kidato cha pili katika Halmashauri kwenye shule za sekondari zikiwemo shule 27 za Serikali na shule 23 za binafsi. Idadi ya watahiniwa wa kidato cha pili kutoka shule zote ni 7990 wakiwemo Wavulana 3917 na Wasichana 4073 wanaendelea kufanya mtihani huo. Pia, tarehe 15/11/2021 hadi 01/12/2021 kutakuwa na mitihani ya kidato cha Nne katika shule za sekondari zilizopo Manispaa ya Ilemela ambapo jumla ya watahiniwa 7,757 watafanya mitihani hiyo.

### 2.4 Taarifa ya Mapokezi wa Fedha za Ujenzi wa Kituo Cha Afya Kayenze na Ujenzi wa Madarasa katika shule za Sekondari.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Halmashauri imeidhinishiwa jumla ya Tsh. 1,940,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 97 katika shule za sekondari. Hadi sasa Halmashauri imepokea jumla ya Tsh 1,840,000,000.00 kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 92 Katika Shule 26 za Sekondari ikiwa ni kupunguza upungufu wa miundo mbinu ya



Scanned with CamScanner

madarasa na kufanya maandalizi ya mapokezi ya Wanafunzi wa Kidato Cha Kwanza Kwa Mwaka 2022. Shule ya sekondari Angeline Mabula ilidhinishiwa Tsh. 100,000,000.00 kujenga madarasa 5 ambapo fedha hizo bado hazijapokelewa. Pia, Tsh 250,000,000.00 zimepokelewa kutoka Serikali Kuu kwa Ajili ya Ujenzi wa Kituo Cha Afya Kayenze. Miundombinu itakayojengwa ni Jengo la Wagonjwa wa Nje, Maabara na Kichomea Taka. Kituo hiki kitajengwa katika Mtaa wa Iponyabugali kata ya Kayenze. Nawaomba viongozi katika ngazi zote kushirikiana vizuri katika kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo.

### 2.5 Taarifa ya kuwaondoa machinga/wafanyabiashara ndogondogo katika maeneo yasiyo rasmi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Hadi kufikia tarehe 04/11/2021Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ilikuwa imefanya zoezi la kuwaondoa wafanyabiashara wadogowadogo (Machinga) wapatao 3187 wakiwemo Wanaume 2345 na Wanawake 842 wakitokana na makundi kama wauza Nguo, Viatu, Bidhaa za urembo, Matunda, Samaki na Vyakula ambao walikuwa wakifanyia biashara katika maeneo yasiyo rasmi na kuwahamishia katika maeneo rasmi ambayo ni Kirumba, Buzuruga, Nyamanoro, Pasiansi, Buswelu, Nyasaka na Kitangiri. Zoezi hili limeenda sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya masoko kama kuweka taa na kujenga Shades. Tunawaomba wafanyabiashara wote na wananchi kuendelea kuwa watulivu kutumia maeneo waliyopangiwa wakati Serikali ikiendelea kufanya juhudi zaidi za kuboresha miundombinu ya kufanyia biashara. Aidha, hatua za kisheria zitachukuliwa kuyalinda mafanikio haya kwa wale watakao kiuka kwani zoezi hili ni endelevu.

### 2.6 Taarifa ya Uzinduzi wa Kampeni ya Usafi na Mazingira katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Uzinduzi wa Kampeni ya Usafi wa Mazingira ulifanyika Tarehe 23/10/2021 na Mhe. Mkuu wa Wilaya ndugu Hasan Masala kwa kushirikiana na viongozi wengine Mstahiki Meya na Mkurugenzi, Wataalam wa Manispaa ya Ilemela pamoja na wananchi walifanya uzinduzi katika Kampeni ya Kufanya Usafi na Mazingira. Zoezi hili lilifanyika katika Kata ya Kirumba ambapo kazi zlizofanyika ni pamoja kufyeka na kuzoa takataka katika eneo la furahisha na eneo la sokoni.



Scanned with CamScanner

**2.7 Taarifa ya kuwajengea uwezo Waheshiwa Madiwani na Watendaji wa Kata.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa kushirikiana na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo ilifanya mafunzo ya siku 5 kuanzia tarehe 6-10/10/2021 katika Ukumbi wa Manispaa kwa lengo la kuwajengea uwezo waheshimiwa madiwani kuwawezesha kusimamia utendaji kazi katika hutoaji wa huduma bora kwa wananachi kwa kuzingatia misingi ya sheria uongozi na utawala bora. Hali kadhalika watendaji wa kata 19 walijengewa uwezo juu ya udhibiti wa fedha, mahusiano baina wananchi na Waheshimwa madiwani, masuala ya manunuzi, Mfumo wa uwekaji Mipango na Usimamizi wa miradi, Majukumu na Madaraka ya Mamlaka ya serikali za Mitaa. Mafunzo haya yalilenga kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi wa viongozi katika ngazi ya Kata na Wilaya.

**2.8 Taarifa ya Uhamasishaji na Uchanjaji wa Chanjo ya UVIKO-19**

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ina vituo 30 vinavyotoa huduma ya chanjo,
Hata hivyo huduma ya chanjo ya kujikinga na homa kali ya virusi vya korona (UVIKO-19) ilianza kutolewa tarehe 03/08/2021. Halmashauri ilipokea jumla Chanjo aina JANSEN 7,600 na waliochanjwa kwa kutumia aina hiyo ya chanjo ni 6147 sawa 96.2%. Aidha, mnamo tarehe 18/10/2021 halmashauri pia, ilipokea tena aina nyingine ya chanjo 9,096 inayojulikana kwa jina la Sinopharm. Hadi sasa chanzo zilizotumika ni 744 sawa na 8.2% na zoezi la uchanjaji linaendelea. Aidha, natoa rai kwa viongozi, Waheshimiwa Madiwani na wananchi kwa ujumla kuendelea kuhamasishana kwa ajili ya kuchanjwa kudhibiti janga hili la UVIKO 19.

Eng. Modest J. Apolinary
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**ILEMELA**



Scanned with CamScanner